# MASIKITIKO YA MUNGU

Nawasalimu katika jina la BWANA; Amani iwe nanyi.

Mungu aliyeziumba mbingu na nchi, bahari pamoja na vyote vilivyomo; Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo; Mungu wa Manabii na Mitume wote ambao kutokana nao, Kanisa la Mungu leo ni uzao wake, alikuwa na mpango wa kuwaumba wanadamu, mpango unaoendelea mapaka sasa. Na madhumuni ya mpango huo ni kuwafanya wanadamu wote kuwa viumbe wa kiroho na kuwa sehemu ya Familia yake ya kiroho, wakitawala si katika Dunia peke yake, bali katika uumbaji wake wote; maana anasema, ***"…Umemvika taji ya utukufu na heshima, Umemtawaza juu ya kazi ya mikono yako; Umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake…" Waebrania 2:7-8.***

Lakini kama tujuavyo kwamba; ili mwanadamu afikie hatua hiyo, ni sharti kwanza afanyike kuwa kiumbe wa kiroho, hatua inayoanzia kwa mwanadamu wa kimwili *{yaani, wa mwili wa damu na nyama};* na hatua ya pili ni kukuza *{kujenga}* nia *{akili/ufahamu}* na tabia ya Mungu ndani yake; na hapa ndipo tulipo hivi sasa kama Kanisa. Tunafahamu kwamba; mwanadamu hakuendelea katika mpango huo wa Mungu, maana alidanganywa na akadanganyika, na hivyo akasalia kuwa kiumbe wa kimwili tu, mwenye kujishughulisha na mambo ya mwili tu *{agiza ujumbe wetu usemao,* ***"MWANADAMU NI NANI?",*** *kwa maelezo ya kina zaidi, na utatumiwa bure ujumbe huo}.*

Kanisa la Mungu ni watu ambao Mungu katika Kristo Yesu amewaita kutoka katika huo udanganyifu wa Shetani na kuanza hatua ya pili ya uumbaji ndani yao ambayo ni kujenga nia *{akili/fahamu}* zao ili ziwe kama yake, na tabia zao pia zifanane na tabia yake ya haki. Ukuaji huu haujikiti *{hauhusiani}* katika mambo ya mwili kama ambavyo watu wengi wanadhania. Mungu aliumba na kukamilisha mwili huu wa damu na nyama pamoja na mahitaji yake yote. Kwa hivyo basi; anachofanya hivi sasa ni kushughulika na mambo ya kiroho peke yake. Baada ya udanganyifu, mwanadamu alianza kufanya mambo yote kulingana na mwili, maana ufahamu wao wote unaishia katika mambo ya mwili tu. Na kwa sababu hiyo; pindi watu *{na hata washirika wa Kanisa ama wale waitwao Wakristo}* leo wanapozungumzia Baraka za Mungu; basi wanafikiria tu juu ya utajiri mkubwa, hadhi *{nafasi}* za juu katika jamii, afya nzuri ya mwili na mengine kama haya.

Lakini Kristo alipoanza kuwafundisha wote walioamini, jambo la kwanza aliloanza nalo ni hili la mawazo ya watu kuelekea katika mambo ya mwili tu ambayo kwa ujumla wake ni ibada ya sanamu. Alianzia katika kiini cha mambo yote *{katika nia au ufahamu}* akisema; ***"Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe…" Mathayo 16:24.*** Baada ya hapo, akaenda mbele zaidi kwa kuwaambia wasiishi tena kwa mtazamo wa Mataifa ambao wanafahamu kwamba maisha *{uhai}* yanategemea tu mahitaji ya mwili; alisema, **"Msisumbuke basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? au Tuvae nini? Kwa maana hayo yote Mataifa** *{waliodanganyika}* ***huyatafuta…" Mathayo 6:31-32.*** Lakini kwa nini alisema hivi? Je! maisha

hayategemei ama kuendelezwa na vitu hivi? Yesu anaendelea kutuweka wazi akisema; ***"…uzima*** *{uhai/maisha}* ***wa mtu haumo*** *{hautegemei}* ***katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo" Luka 12:15.*** *{Agiza ujumbe wetu usemao,* ***"THAMANI YA UKRISTO",*** *kwa maelezo zaidi juu ya hili}.*

Sasa basi wapendwa; ikiwa tutaondoa wasiwasi huu katika nafsi zetu, na pia tukaondoa mtazamo tuliokuwanao dhidi ya vitu vinavyotuzunguka *{mahitaji};* tutabakiwa na nini sasa, na ni kwa namna gani tunaenda katika mafunzo? Kile kilichopo katika nia ya Mungu hivi sasa, ni kumfanya mwanadamu kuwa kama yeye kwa madhumuni ya kurithi na kutawala katika ufalme wake; na hiki ndicho ambacho Kristo anasema kwamba, tunapaswa kukipigania. Tafadhali sikia kile anachotuambia; anasema, ***"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo*** *{mahitaji ya mwili}* ***yote mtazidishiwa" Mathayo 6:33.***

Lakini sasa, ni kwa namna gani? Hapa ndipo ambapo siri ya uongo *{udanganyifu}* ilipo, na ndipo ambapo Mungu anapasikitikia hivi sasa. Nia na tabia ya maisha yale ambayo Mungu katika Kristo Yesu analiambia kanisa ni yale ambayo akili *{nia/ufahamu}* ya mwanadamu haiwezi kuyafahamu. Tunafahamu kwamba akili ya mwanadamu inafahamu mambo kwa kuona, kusikia, kuonja, kunusa na kuhisi *{yaani, kwa kutumia milango mitano ya fahamu}.* Lakini maisha yale ambayo Mungu analifundisha Kanisa, ambayo ni ya ***"ulimwengu ule ujao tunaounena {Waebrania 2:5}",*** ni mfumo wa maisha ambayo milango mitano ya fahamu za mwanadamu haziwezi kuufahamu; maana ni ***"mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao" 1 Wakorintho 2:9.*** Sasa basi, tutayafahamuje hayo maisha ili tuanze kuyaishi? Mungu alilifahamu jambo hili vizuri sana, na hapa ndipo kazi ya Roho Mtakatifu inapohitajika; na roho huyo anakuwa kwetu mlango wa sita wa fahamu; maana Bwana wetu anasema; ***"Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho*** *{si kwa utajiri wala elimu ya juu ya kimwili}****…makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu", soma 1 Wakorintho 2:10-12.***

## MBINU ZA AJABU

Wapendwa; inasikitisha kuona aina ya mahubiri *{kwa madhumuni ya kuwavuta watu kwa Kristo}* ambayo jamii kubwa sana ya makanisa wanahubiri, hasa wale viongozi wakuu; na hili ndilo ambalo linamsikitisha *{linamhuzunisha}* sana Mungu! Na hili ninalisema kama mmojawapo wa wale ambao Mungu amewatuma kuhubiri; na unaweza kulithibitisha hili kwa maandiko ikiwa unahitaji kujua. Tunafahamu sote kwamba; ni Kristo ndiye awachaguaye watu; tena ni wale waliovutwa *{waliopelekwa}* kwake na Mungu mwenyewe; maana anasema, ***"Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi…" Yohana 15:16.*** Na je! ni wapi uchaguzi huo unapoanzia? Anaendelea kufafanua akisema; ***"Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka*** *{aliyenituma}****…" Yohana 6:44.*** Hii ina maana kwamba; si jitihada wala umakini wa mtu, isipokuwa ni kutokana na Mungu mwenyewe kupitia

kwa neno lake kunakoweza kumfanya mtu kuamini na kufanyika kuwa mshirika wa kanisa. Ni Mungu peke yake kwa njia ya roho wake *{kama tulivyoona}* awezaye kumpa mtu kufahamu. Kwa wale wote ambao Mungu anawaita, Kristo anasema; ***"Kondoo wangu waisikia** {waijua}* ***sauti yangu…" Yohana 10:27.***

Tunafahamu sote kwamba sauti ya Kristo ni Maandiko ya Mungu. Na hii ndiyo maana anatuambia kwamba, tukitaka kumfahamu mjumbe wake aliyemtuma; basi tutamfahamu kwa neno *{maandiko},* maana, ***"…yeye aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu…" Yohana 3:34.*** Na mara baada ya kuyazungumza maneno ya Mungu, mtumwa *{mjumbe}* wake haendelei zaidi kwa kuwashawishi watu ili waamini, maana wanaamini kwamba mwalimu wao *{yaani Kristo}* anawaambia kwamba, ***"Yeye aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu" Yohana 8:47.*** Wapendwa; kazi ya kuihubiri injili ni rahisi kiasi hicho; yaani ni kuongea ukweli tu ambao wewe mwenyewe pia uwe unaishi kwao; kisha, ngojea kuona kwamba ni nani ambaye Mungu atamvuta kwa Kristo kuwa kanisa.

Inasikitisha kusema kwamba; sehemu kubwa ya wale wanaoonesha kuihubiri injili hivi sasa wamekuja *{wameibuka}* na mbinu iliyo tofauti sana ambayo kwa sehemu kubwa imeizika injili ya Kristo na kuifanya ionekane kama takataka na unafiki tu! Katika jitihada za kujipatia wafuasi; ndugu zetu wa Kimataifa *{Wazungu}* wamefanya kazi ya injili katika bara la Afrika, na hasahasa katika nchi ya Kenya; si kwa sauti ya Kristo *{ambayo ni maandiko},* bali kwa utajiri wao na kulifanya agizo la Mungu lisemalo, ***"utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo** {mahitaji}* ***yote mtazidishiwa",*** kugeuzwa na kuwa, ***"yatafuteni kwanza mahitaji ya mwili, na kisha ufalme wake, na haki yake; mtazidishiwa".***

Kwa upande mwingine; wahubiri wazawa *{yaani, Waafrika wenzetu},* wao pia katika jitihada za kutafuta kuwa na wingi wa watu wanaowazunguka; wameiweka injili kando, ama kuizamisha majini isionekane, ili watimize haja yao ya kupata idadi kubwa ya watu wanaowafuata, na hivyo wakaanza kuhubiri kile ambacho watu wanataka kukisikia. Kwa hivyo, hawa wahubiri wa Kimataifa wanashirikiana na hawa wahubiri wazawa na kuja kama kanisa la Mungu, katika namna ya kutoa misaada kwa watoto yatima, wajane na wenye mahitaji mbalimbali ya kimwili, wakiwaahidia misaada na kutimiza ahadi zao kwa wale wanaowafuata. Hawana tofauti kabisa na Mashirika ya kijamii yafanyavyo. Na kwa hali hiyo mpaka sasa, si wengi kati ya wale wanaolifahamu kanisa la Mungu nchini Kenya *{na hata nchi nyingine za jirani kama Tanzania n.k.}* wanaoweza kulitofautisha na mashirika ya misaada ya kijamii *{yaani, NGOS}.* Lakini si jambo jipya, maana hata wakati wa Kristo pia yalitokea kama haya; bali Kristo hakuyanyamazia, na aliwaambia; ***"Ninyi mnanitafuta, si kwa sababu mliona ishara, bali kwa sababu mlikula ile mikate mkashiba" Yohana 6:26.***

Na kama ninyi ndugu zetu wa Kimataifa mnataka kuthibitisha ikiwa Mungu anajishughulisha na jambo hili; basi ni muhimu kwenu kufanya uchunguzi wa kina na kwa kuomba sana; kwa sababu ninafahamu kila kundi lina uwakilishi wake hapa Afrika. Kile ninachokitoa hapa ni mwanga *{au dokezo}* tu. Lakini ikiwa mnadhani kwamba uwakilishi wenu

ni wa kweli na unatosha *{ila mniwie radhi kwa kuyasema haya},* wachunguzeni na mtakuta kwamba, ni asilimia mbili *{2%}* tu ama chini ya hapo wanaosoma kile mnachotuma kama ujumbe *{masomo},* na ambao wanadai kuwa ni mzuri na wenye kuwavutia wengi wa waaminio; na wachache zaidi, chini ya silimia hiyo ndiyo wanaoelewa kile wanachokisoma. Naam; ikiwa wawakilishi wenu ni watu wanaomcha *{ama wanaomwogopa}* Mungu na si wanaotafuta kuwapendeza wanadamu; basi watawadhibitishieni haya ninayoyaelezea hapa. Kile mlichozoea kupokea kutoka kwa wawakilishi wenu ni kusikia mkiambiwa jinsi ambvyo mahubiri yenu ni mazuri na yanawavutia watu wengi. Lakini je! mmewahi kusikia hata mmoja akizungumzia kiini cha ujumbe na kuuelezea uzuri wake zaidi tu ya kusifia kwamba ujumbe ni mzuri?

Kwa wale ambao mmekuwa na nafasi ya kuwatembelea; mmewaona wangapi na mara ngapi wakishiriki kwa dhati katika mafundisho ya biblia, wakijaribu kujifunza ukweli? Mtakubaliana nami kwamba, kile mnachokipata kwa wingi ni mahitaji ya kifedha tu. Mara baada ya kuambiwa kwamba ujumbe wenu ni mzuri; basi kinachofuata ni baadhi yao kuwaambia kuwa hitaji la makundi mengi ni kutaka kupata Biblia na pia kutembelewa. Na baada ya hapo, mahita zaidi yanafuata kama vile msaada kwa mayatima, wajane, fulani anakabiliwa na njaa, kuboreshewa makazi na mengine mengi kama haya. Hivi vyote ni vitu vya kimwili tu visivyoweza kumsaidia mtu kuyafahamu mambo ya kiroho!

Ukweli kuhusu watu hawa mnaojipatia kama wafuasi ni huu; wengi wa watu hawa si kwamba hawafahamu lo lote kuhusu injili tu, bali hawana hata ile haja ya kuyafahamu maisha ya Mungu! Na hii ni kwa sababu, hawakupitia katika hatua ya kwanza ambayo ni kuvutwa kwa injili *{kwa neno},* bali wao walivutwa kwa fedha. Na hawa ndio watu ambao ninyi mnapoteza zaka ya Mungu kwa kuwahudumia huku mkidhani ya kuwa mnalisaidia kanisa. Siwalaumu ninyi kwa sababu, kutokana na umbali mliopo, hamyafahamu yale yanayofanyika huku. Kwa hivyo, ninachofanya ni kuwasilisha kwenu zile hisia ambazo Mungu ameziweka ndani yangu, na ambazo ni masikitiko yake; kuweka bayana *{wazi}* siri ya uasi ambayo ninyi mnaisaidia kwa kutofahamu kwenu, na hivyo kwamba mwache mara moja kutumiwa bila kujua na kushindwa kulisimamia kanisa na injili yake katika ukanda huu kwa kushirikiana na wadanganyifu ambao kwa hao, ***"njia ya kweli inatukanwa. Na katika kutamani wanajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa…" 2 Petro 2:2-3.***

Nukuu hili tafadhalini, ili msije kunielewa vibaya. Kamwe sijaribu kutaka kuwavuta ninyi ili mshirikiane nami. Sijajitokeza kutafuta washirika katika mwisho huu. Lakini pamoja na hayo; nafahamu kwamba Mungu anao watu wenye nia kama yangu ndani yao, na pindi watakapoisoma tahadhari hii, atawapa kufahamu, na ikiwa kuna uhitaji, atatuunganisha pamoja katika kazi ya koroho. Lakini hicho si kile ninachokitazamia hapa. Kwa hivyo, hebu mtu asinifikirie kama mfanyabiashara *{au mtafutaji}.* Ni Mungu ndiye afanyaye kazi ya kuwavuta watu katika kweli yake. Nimeonywa na Kristo, na hivyo nikiwa kama ***"mtumishi wake, na wakili wa siri za Mungu" {1 Wakorintho 4:1};*** ninawajibika kuuweka ukweli mezani mbele yenu. Ni juu yenu kuhukumu kile nisemacho, na si kwa ***"hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki" Yohana 7:24.***

Na hivyo basi wapendwa; jueni na fahamuni kwamba; mwenendo huu unapiga vita injili huku. Lakini ninamshukuru Mungu kwa sababu kama ilivyo; wale wote walio wake wanaendelea kuisikia sauti yake na kuvutwa nje ya udanganyifu wa ibada ya sanamu. Bila kujua kile ambacho mnajishughulisha nacho, lakini kwa wakati huo huo mkisisitiza kuwa kuna mmoja anayefuata maagizo yenu; mnamtuma kutafuta watu, mkidhani mnalilisha kanisa. Wakati aendapo kuwahubiria; kwa kuwa kile kinachowavuta kwenu si injili; basi pindi awahubiripo, watu wote husinzia tu! Na mara baada tu ya mahubiri kumalizika, wanafahamu kwamba kile kinachofuata sasa ni kupokea kile ambacho mzungu/wazungu wameleta kama misaada! Kwa hivyo, kila mmoja anaamka na kukaa makini kabisa. Na endapo mjumbe wenu ataonekana pasipo msaada wo wote ule kwao; basi wazo la kwanza linalopigana katika nia *{akili}* zao ni kwamba, **"Amekula pesa zetu!".** Naamini mmepokea tuhuma na lawama nyingi sana juu ya swala hili. Hebu sasa oneni mnayoyafanya! Mnamshurutisha mtu kufanya ushirika na wasioamini ilimradi tu awapendeze ninyi, na hii ni kwa sababu hamchunguzi kwamba ni nani ambaye Mungu anamtumia kuusimamisha ukweli mahali fulani. Je! halazimiki mtu huyo kumpuuza Kristo kwa sababu ya kufikiria kwenu tu? Na kwa njia hiyo je! ninyi hampigani na Kristo pamoja na injili yake?

Haya yote yametokea kwa sababu kamwe hatukufuata maagizo ya Kristo katika kuifanya kazi yake. Katika kuyafanya hayo, hatukuwa tukiihubiri injili. Lakini bado hatujachelewa. Hii ndiyo maana Mungu katika Kristo Yesu amelileta jambo hili mbele yetu hivi sasa ili muwe makini na kwamba mpate kuzirekebisha njia zenu. Agizo la Kristo ni **"kwanza ufalme wa Mungu na maisha yake** *{haki yake},* **na ndipo baada ya hapo, wote waaminio wanaweza kusaidiwa katika mahitaji ya kimwili *{soma Yakobo 2:15-16; Mathayo 6:33}.*** Hivi ndivyo tunavyopaswa kuifanya kazi ya Mungu. Kazi yenu inawavutia watu wa kidunia ambao ***"mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani" Wafilipi 3:19.***

Wapendwa; kwa sababu ya haya, sisi ambao tunahubiri ufalme wa Mungu na haki yake, tunapata wakati mgumu sana kuwashawishi watu hawa kwamba, ***"ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu" Warumi 14:17.*** Ikiwa kweli ninyi ndugu mnaieneza injili ya kweli; basi jueni na fahamuni pia ya kuwa Mungu amemwinua mtumishi wake katika ukanda huu wa dunia, ambaye ikiwa kweli ninyi mnaongozwa na roho mtakatifu, mtalithibitisha hili kama tulivyoona ***{tafadhali soma tena Yohana 3:34; 8:47}.*** Hii ni nguzo ambayo mnapaswa kuitumia katika kuifanya kazi huku. Sisi ndugu wa Kiafrika, tunawafahamu washirika wetu wa kiafrika vizuri sana zaidi yenu; vile vile kama ambavyo ninyi pia mnavyowafahamu washirika walioko huko kwenu vizuri sana zaidi yetu. Na hii ndiyo maana Mungu ameona vema awe na watumishi wake aliowachagua katika ukanda huu pia ili kwamba mpate kuwasiliana nao katika muunganiko wa kiroho katika kazi yake. Kumbukeni; Mungu hana upendeleo. Anaweza kumfanya ye yote kuhudumu kwa uwezo ule ambao yeye Mungu mwenyewe atakusudia.

Haya ndiyo masikitiko ya Mungu, na yuko hapa hivi sasa akiyaweka mbele yenu. Ninamshukuru sana kwa sababu ya upendo wake mkuu alionao kwetu. Na ndiyo sababu

iliyomfanya ayafunue wazi haya maelekezo kwa ye yote yule atetemekaye pindi alisikiapo neno lake. Ninayanena yote haya kutoka kwa Mungu Baba yetu, na katika Kristo Yesu Bwana wetu kwa watumwa wake. Je! wewe ni miongoni *{mmoja}* mwao?

Jambo la mwisho; tafadhalini kumbukeni kwamba, zile zaka mnazotumia si zaka zenu kiasi kwamba mzitumie kama mpendavyo wenyewe. Mungu wetu anasema; ***"Kwa kuwa zaka ya wana wa Israeli, waisongezayo kuwa sadaka ya kuinuliwa kwa BWANA*** *{na kuanzia hapo ni ya Mungu, si yetu},* ***nimewapa*** *{Mungu mwenyewe, si ninyi}* ***Walawi kuwa urithi wao…" Hesabu 18:24.*** Sasa basi; ni juu ya kila mmoja kutambua ni nani aliye mtumishi wa kweli na aliyechaguliwa na Mungu ambaye atapokea zaka yake. Msipokuwa makini na kumpa ye yote mtakayemchagua ninyi wenyewe; basi ni juu yenu na Mungu na wala sisi hatuhusiki tena hapo. Baada ya kuwa mmepaimarisha pa kulipa zaka zenu, mahali ambapo Mungu amelikalisha jina lake *{hekalu lake},* basi kazi yenu inaishia hapo. Hamna sehemu tena katika kupanga matumizi yake, maana Bwana wetu anasema; ***"Lakini hawakuulizwa habari ya ile fedha waliyokabidhiwa; maana walitenda kazi kwa uaminifu" 2 Wafalme 22:7.***

Hebu basi; wale wote watakaopewa kuifahamu sauti hii, na wayachukue mawaidha haya kwa umakini mkubwa na kuzisahihisha njia zao. Hebu na tujinyenyekeze kikamilifu kwa Mungu na kumruhusu atuongoze ko kote atakako. Hebu pia tumruhusu kuifanya kazi yake ndani yetu kulingana na mapenzi yake. Hebu na tujikane nafsi zetu na kumruhusu auoneshe ulimwengu tofauti iliyopo kati ya maisha yake na yale maisha ya ulimwengu. Neema ya Mungu na iwe pamoja na Israeli wa Mungu.


**Ni watumwa wa Mungu wanazungumza nawe kupitia kwa :-**

**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Nambari za simu; +255 753 359 179, +255 688 359 179 na +255 655 659 179.**

**Barua pepe; Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg**

**NA**

**KANISA LA MUNGU – KENYA**

**Barua pepe; endcog@gmail.com**